JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA TEMEKE

Baruapepe: temekerh@afya.go.tz, S.L.P 45232 Dar es Salaam, Simu 0222856007


Kumb. Na.TRRH/IMF COVID 19/02 Tarehe: 10/12/2021

# MKATABA WA KAZI

**KATI YA**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE**
**S. L. P 45232, DAR ES SALAAM**
***("MWAJIRI")***

**NA**

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI POLISI (T)**
**S.L.P 79429, DAR ES SALAAM**
***("FUNDI")***

**KWA AJILI YA**

**UKARABATI WA JENGO LA EMD**
**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE**

**ME/0007/W/2021-2022/TMKRRH/LOT 002**

# FOMU YA MKATABA

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 10 Mwezi Disemba, 2021 Kati ya Hospita Ya Rufaa Ya Mkoa Temeke(Hapa ataitwa "Mwajiri") kwa upande mmoja na ShirikaLaUzalishaji Mali Polisi (T) (Hapa ataitwa "FUNDI") kwa upande mwingine.

Kwa kuwa Mwajiri anataka kazi zifanyike yaani: *UKARABATI WA EMD* kwa bei ya Mkataba wa shilingi za Tanzania ***Milioni thelasini na nane laki nane na elfu hamsini tu (Tshs. 38, 850,000 /= Bila VAT)*** na kwa barua ya kukubali yenye Kumb Na. **TRRH/IMF COVID 19/02** ya tarehe **03/12/2021** Ilikubali Nukuu ya Bei ya Fundi kwa utekelezaji na ukamilishaji wa kazi hiyo.

**SASA MKATABA HUU UMESHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO:**

1. Katika Mkataba huu maneno na maelezo yatakuwa na maana sawa kama yalivyopewa katika Masharti ya Mkataba unaorejelewa na;
2. Nyaraka zifuatazo zitachukuliwa kwa pamoja na zisomeke na kufasiriwa kuwa ni sehemu ya Mkataba huu, yaani;
    1. Fomu ya Mkataba:
    2. Barua ya Kukubali Nukuu ya Bei:
    3. Fomu ya Kuwasilisha Nukuu ya Bei:
    4. Masharti Maalumu ya Mkataba:
    5. Masharti ya Jumla ya Mkataba:
    6. Michoro:
    7. Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi:
    8. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, tamko dhidi ya rushwa).

3. Nyaraka zote zilizotajwa hapo juu zitarejelewa hapo kama 'Mkataba' na zitachukuliwa kuwa zinakamilishana na zinajieleza sawa lakini ukitokea utata au uhitilafiano zitakuwa na umuhimu katika mfuatano wake kama zinavyoonyeshwa hapo juu.

4. Katika kuzingatia malipo yanayofanywa na Mwajiri kwa Fundi kama baadaye inavyotajwa, Fundi hapa anakubaliana na Mwajiri kutekeleza na kukamilisha kazi kwa kufuata makubaliano, kwa hali zote kulingana na vifungu vya mkataba.

   Mwajiri hapa anakubali kumlipa Fundi kwa kuzingatia utekelezaji na ukamilishaji wa kazi, jumla ya fedha za Tanzania kwa bei ya Milioni thelasini na nane laki nane na elfu hamsini tu (Tshs. *38, 850,000*/= Bila VAT) na baadaye imerejelewa kama 'Bei ya Mkataba kwa nyakati na namna iliyoelezwa katika mkataba.

KATIKA KUSHUHUDIA, pande hizi zimekubaliana na kutia sahihi na muhuri katika siku na mwaka kama ulivyoandikwa hapo juu.

| KWA NIABA YA MWAJIRI<br>HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE,<br>S. L. P 45232, DAR ES SALAAM | KWA NIABA YA FUNDI:<br>SHIRIKALAUZALISHAJI MALI POLISI (T),<br>S. L. P 79429, DAR ES SALAAM |
|---|---|
| Sahihi: ………………………………<br>Jina: Dr.Joseph Kimario<br>Cheo: Mkurugenzi<br>Tarehe: 10/12/2021<br>Muhuri: MGANGA MFAWIDHI S. L. P. 45232 DAR-ES-SALAAM HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA TEMEKE | Sahihi:<br>Jina: FRANCIS D. SUKA – SSP<br>Cheo: DoP<br>Tarehe: 10 DECEMBER, 2021<br>Muhuri: For: EXECUTIVE DIRECTOR TANZANIA POLICE FORCE CORPORATION SOLE P. O. Box 79429 DAR ES SALAAM |

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA TEMEKE

Baruapepe: temekerh@afya.go.tz, S.L.P 45232 Dar es Salaam, Simu 0222856007

# MWALIKO WA KOTESHENI

## KWA AJILI YA

## UKARABATI WA JENGO LA EMD KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE

KOTESHENI Na: ME/007/W/2021-2022/TMKRRH/LOT 02.

NOVEMBER, 202

## Dibaji

Ununuzi wa kazi ndogo ndogo za ujenzi zilizo chini ya miradi inayogharimiwa na Umma unafanywa kulingana na sera na taratibu zilizowekwa chini ya sheria ya Ununuzi katika Sekta ya Umma Na.7 ya Mwaka 2011 na Kanuni za Ununuzi katika Sekta ya Umma (Kazi, Bidhaa, Huduma Zisizohitaji Ushauri wa Kitaalamu na Uuzaji wa Mali za Umma kwa Zabuni)- Tangazo la Serikali Na. 446 la Mwaka 2013 Marekebisho ya Mwaka 2016 na Kanuni za Bodi za Zabuni za Mamlaka za Serikali za Mitaa (Uanzishwaji na Utendaji) - Tangazo la Serikali Na. 177 la Mwaka 2007 ( zote zitaitwa Kanuni za Ununuzi katika Sekta ya Umma).

Mwaliko huu Sanifu wa Kotesheni (MSK) wa Ununuzi wa kazi ndogo ndogo umetayarishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi katika Sekta ya Umma (MUUU) kwa ajili ya kutumiwa na Taasisi Nunuzi (TN) wakati wa ununuzi wa kazi ndogo ndogo za ujenzi.

Taratibu zilizoainishwa katika nyaraka hizi ni lazima zitumike katika miradi ya umma ambayo gharama zake zote au sehemu ya gharama hulipwa kwa fedha za Umma kulingana na masharti ya Sheria ya Ununuzi katika Sekta ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake.

Kwa taarifa zaidi juu ya ununuzi chini ya miradi inayogharimiwa na fedha za umma, tafadhali wasiliana na:


Ofisa Mtendaji Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi katika Sekta ya Umma,
S.LP. 49,
Dar es Salaam

**Simu: 2121236/7, 2133466**
**Faksi: 2121238**
**Barua pepe: ceo@ppra.go.tz**

Tovuti: http://www.ppra.go.tz

## Vifupisho

| | | |
|---|---|---|
| GCC | : | General Conditions of Contract - Masharti ya Jumla ya Mkataba – MJM |
| GPN | : | General Procurement Notice –Tangazo la Jumla la Ununuzi -TJU |
| IFQ | : | Invitation for Quotation Mwaliko wa Kotesheni (Zabuni Ndogondogo)MK |
| NCB | : | National Competitive Bidding – Ushindani Zabuni Kitaifa - UZT |
| PE | : | Procuring Entity - Taasisi Nunuzi - TN |
| URT 2011 | : | Public Procurement Act No. 7 of 2011 - Sheria ya Ununuzi katika Sekta ya Umma Na. 7 ya 2011 Kanuni 2013 Marekebisho ya Mwaka 2016 |
| BOQ | | Bill of Quantities - Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi – MMK |
| SCC | : | Special Conditions of Contract - Masharti Maalumu ya Mkataba -MMM |
| SIFQ | | Standard Invitation for Quotation - Mwaliko Sanifu wa Kotesheni - MSK |

# SEHEMU I: MWALIKO WA NUKUU ZA BEI (ZABUNI NDOGONDOGO ZA UJENZI)

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA TEMEKE**

**Baruapepe: temekerh@afya.go.tz, S.L.P 45232 Dar es Salaam, Simu 0222856007**


Tarehe: 23/11/2021

# TANGAZO

## MWALIKO WA ZABUNI YA KUMPATA FUNDI MCHUNDO/ MKAZI WA KUKARABATI JENGO LA ICU KATIKA HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE ILIYOPO WILAYA YA TEMEKE ME/007/W/2021-2022/TMKRRH/LOT 02

1 Mwaliko huu wa Zabuni kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la ICU katika hospital ya rufaa ya mkoa Temeke iliyopo Wilaya ya Temeke kwa mwaka wa fedha 2021 - 2022

2 Unakaribishwa kuja kuchukua kabrasha la zabuni katika Ofisi ya Mkurugenzi wa hospitali

3 Unakaribishwa kuleta Nukuu yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (MMK) uliofafanuliwa katika sehemu ya II ya nyaraka hiyo

4 Zabuni zote katika uhalisia wake (original) na nakala moja (1) zilizojazwa kwa usahihi na kuwekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa Jina na Namba ya zabuni, na ziwasilishwe ofisi ya Mkurugenzi wa Hospitali kabla ya siku ya mwisho ya kuwasilisha.

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Zabuni ni Alhamisi tarehe **25/11/2021** kabla ya *Saa nane kamili (8:00) Mchana.* Zabuni zitafunguliwa mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wazabuni/ wawakilishi watakaoamua kuhudhuria katika ufunguzi wa Zabuni hii

6 Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa Zabuni, hazitakubaliwa kwa ajili ya kutathminiwa kwa hali yoyote ile.

……………………………………………

MKURUGENZI

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA TEMEKE

SEHEMU II: MCHANGANUO WA GHARAMA ZA UFUNDI

## MCHANGANUO WA GHARAMA ZA UFUNDI KWA UKARABATI WA JENGO LA EMD

| No. | KAZI ZITAKAZOFANYIKA | GHARAMA |
|---|---|---|
| 1 | Kuvunja baadhi ya kuta, kuezua paa na kenchi zake, kutindua sakafu, kuondoa milango na fremu zake | 2,000,000 |
| | **BOMA** | |
| | Kujenga kuta pamoja na kuweka karatasi ya kuzuia unyevunyevu (DPC) na kuweka venti | 4,000,000 |
| | Kujenga mkanda wa juu (ring beam- kuchanganya na kumwaga zege kwa kutumia mashine, kusuka nondo, kufunga na kufungua mbao | 1,500,000 |
| | **MILANGO** | |
| | Kuweka fremu za milango, kufunga top, kuweka vitasa, kioo kwenye vent pamoja na kusawazisha ukuta baada ya kupachika milango | 750,000 |
| | **MADIRISHA** | |
| | Kuweka madirisha ya Aluminium pamoja na grill zake pamoja na kusawazisha ukuta baada ya kupachika madirisha | 1,500,000 |
| | **PAA** | |
| | Kupaua (Kufunga mtambaa panya, kutengeneza na kuweka kenchi na [illegible]) pamoja na fishabodi | 6,500,000 |
| | **KAZI ZA UMALIZIAJI (FINISHING)** | |
| | Kupiga plasta kwenye kuta (ndani na nje) | |
| | Kupiga ripu kwenye kuta nje | 2,000,000 |
| | Kufanya skimming kwenye kuta na dari (ndani na nje) | 2,000,000 |
| | Kujenga sakafu (Epoxy) ndani na kwenye baraza pamoja na tiles kwenye kuta vyoo | 2,000,000 |
| | [illegible] ndani na nje | 3,000,000 |
| | Kufunga "gypsum" kwenye dari pamoja na conice | |
| | Kufunga PCV na reli zake | 1,500,000 |
| | | 400,000 |
| | **RANGI** | |
| 15 | Kupaka rangi kwenye kuta (ndani na nje) | 2,300,000 |
| 16 | kupaka rangi kwenye dari | 1,000,000 |
| | Kupaka rangi kwenye "fascia board" | 400,000 |
| | Kupaka "varnish" kwenye milango na rangi kwenye grill za madirisha | 300,000 |
| | **MFUMO WA UMEME** | |
| | [illegible] na kutandaza bomba za umeme kwenye kuta pamoja na kuweka maboksi ya swichi na kufunga Earth Rod | 2,000,000 |
| | Kutandaza nyaya za umeme katika jengo zima na kufunga taa pamoja na vitaa vyote (ifanywe na fundi umeme) | 1,000,000 |
| | **MFUMO WA MAJI** | |
| | Kuchimba na kutandaza bomba za maji safi na maji taka ukutani na sakafuni | 1,000,000 |
| 22 | Kufunga sanitary appliances kama vile masinki ya kunawia n.k | 700,000 |

K.n.y: MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA POLISI (T)
S.L.P 79429
DAR ES SALAAM

MUNICIPAL ENGINEER
TEMEKE

| | |
|---|---|
| | |
| MAKARO YA MAJI MACHAFU | |
| Kuchimba na kujenga chemba zote | 3,000,000 |
| | |
| JUMLA YA GHARAMA ZA UFUNDI (TSHS) | 40,850,000/= |
| | |

*NB: Kazi zote za zege, ripu na kuta lazima zimwagiliwe maji kwa muda usiopungua siku saba.*

...mashine

K.n.y: MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA POLISI (T)
S. L. P 79429
DAR ES SALAAM

MUNICIPAL ENGINEER
TEMEKE

## SEHEMU III: MAELEKEZO KWA MWOMBAJI

1. Eneo la kazi litakuwa Hospiatali ya rufaa ya mkoa Temeke na kazi inapaswa kukamilika ndani ya ***Siku (60)*** baada ya kotesheni kukubaliwa, Unashauriwa kukagua eneo kabla ya kujaza nukuu ya bei.

2. Katika Nukuu ya Bei ya Mwombaji(Fundi Mkazi) anatakiwa aambatanishe nyaraka zifuatazo;

   2.1 Bei ya Mwombaji iliyojazwa kikamilifu na kutiwa sahihi kulingana na Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi (Lazima ijazwe kikamilifu)
   2.2 Leseni Halali ya Biashara (Kama Fundi Anayo)
   2.3 Cheti cha TIN (Kama Fundi Anayo)
   2.4 Cheti cha CRB/VETA (Kama Fundi Anayo)
   2.5 Orodha Kazi/Mikataba Mitatu (3) ya Majengo ya Serikali/Umma iliyofanywa kama Fundi Mkazi (Local Fundi) kwa kipindi cha hivi karibuni kuanzia 2015 - 2021 pamoja na Majina na Anwani za Waajiri kwa ajili ya kuthibitisha. (Lazima ambatanishe)
   2.6 Cheti cha kusajili kwa kampuni kutoka BRELA(Kama Fundi Anayo)
   2.7 Taarifa za kibenki ikiwa ni pamoja na kuonyesha Majina kamili anayotumia, Akaunti Namba, Tawi la Benki na Benki husika.( Kama anazo)
   2.8 Barua toka kwa Mtendaji wa Mtaa pamoja na Picha mbili za rangi za hivi karibuni iliyopigwa muhuri wa Mtendaji wa Mtaa. (lazima ziambatanishwe)
   2.9 Hatulazimiki kuchukua bei kubwa au ndogo.
   2.10 Unaweza kuchukua vitabu zaidi ya kimoja lakini kazi utapewa moja tu ukiwa na vigezo.

3. Taarifa za maelezo ya mahitaji, viwango na vipimo (Specifications) na Michoro vimeambatishwa kama **Sehemu ya VI na Sehemu VII** kwa mfuatano huo.

4. Bei ya Zabuni;

   4.1 Mkataba utakuwa kwa gharama za Fundi Mkazi
   4.2 Masahihisho kama yatakuwapo, yatafanywa kwa kukata kwakalamu ya wino na kuandika upya, kusaini, kuweka herufi za mwanzo za jina na tarehe.
   4.3 Kiwango kinachotajwa na Fundi Mkazi hakitabadilika katika kipindi chote cha mkataba na hakitafanyiwa marekebisho ya bei kwa sababu yoyote ile isipokuwa kama kuna mabadiliko ya ramani na marekebisho yatakayoridhiwa na Mhandisi Msimamizi wa Mradi.
   4.5 Bei inapaswa kutolewa katika Shilingi za Tanzania.

5. Fundi Mkazi atakamilisha kujaza fomu ya kuwasilishia Nukuu za Bei ambayo imeambatishwa kama**Sehemu VIII**. Fomu ya kuwasilishia bei ni lazima ijazwe kikamilifu bila kubadili chochote katika muundo wake na hakuna fomu mbadala itakayokubaliwa.

6. Malipo yatafanywa kwa Shilingi za Tanzania.

7. Nukuu za bei itabaki kuwa halali kwa kipindi kisichopungua siku 45 baada ya siku yamwisho ya kuwasilisha Nukuu za Bei.

8. Nukuu za bei Mbadala *["hazikubaliki"]*

9. Nukuu za Bei/Kotesheni itakamilishwa na kutiwa sahihi na Fundi Mkazi.

10. Taasisi Nunuzi itatathmini na kulinganisha Nukuu za Bei/Kotesheni kwa namna ifuatayo;

    10.1 Upimaji wa awali; ili kuamua ni kotesheni zipi zenye kutimiza masharti ya zabuni (substantially responsive quotations). Kwa mfano zipi; zimetiwa sahihi vizuri na zimetimiza masharti na maelezo ya mahitaji, viwango na vipimo.

    10.2 Nukuu za Bei/Kotesheni zinazotimiza masharti ya zabuni ya awali zitaangaliwa kama kuna makosa ya kimahesabu. Ikitokea kuna hitilafu yo yote ya kimahesabu kati ya kizio na kiasi kilichotajwa, hapo kizio ndicho kitazingatiwa kwa ajili ya tathmini ya kotesheni na hatimaye kwenye makubaliano ya mkataba.

    10.3 Kulinganisha Nukuu za Bei/kotesheni; katika tathmini ya kotesheni, Kamati ya Tathmini itaainisha kwa kila kotesheni bei ya kotesheni iliyofanyiwa tathmini kwa kurekebisha bei kama ifuatavyo:

    (a) Kufanya marekebisho ya makosa yoyote kama yapo isipokuwa jumla ya fedha zilizotengwa kwa kazi maalumu ambazo matumizi yake huamuliwa na mwajiri (provisional sums) kama ipo , fedha ya dharura katika Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi lakini ikijumuisha kazi za siku iwapo bei zilikuwa na ushindani.

    (b) Kufanya marekebisho yafaayo kwa mabadiliko yoyote yale yanayokubalika, mikengeuko au kusahaulika katika kuingizwa kwenye bei ya jumla;

    (c) Kufanya marekebisho yafaayo kuakisi punguzo au marekebisho mengine ya bei yaliyotolewa.

11 **Taasisi Nunuzi** itatoa mkataba kwa Fundi Mkazi ambaye Nukuu za bei/kotesheni yake imeamuliwa kuwa inatimiza matakwa ya nyaraka za uzabuni na ametoa kotesheni iliyotathminiwa kuwa ya bei ya chini kabisa (lowest evaluated price).

12. **Taasisi Nunuzi** inahodhi haki wakati wa kutoa mkataba kuongeza au kupunguza hadi asilimia 15 ya idadi ya kazi ambazo zilibainishwa hapo awali katika Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi bila mabadiliko yoyote ya bei ya kima cha kizio au masharti mengine na hii itaonyeshwa kwenye fomu ya mkataba.

13. Licha ya yaliyotajwa hapo juu, **Taasisi Nunuzi** inahodhi haki ya kukubali Nukuu ya Bei/Kotesheni yoyote na kukataa kotesheni zote wakati wowote kabla ya kutoa mkataba.

14 Fundi Mkazi ambaye Nukuu ya bei yake imekubaliwa atajulishwa na **Taasisi Nunuzi** kuwa amekubaliwa kupewa mkataba kabla ya kwisha kipindi halali cha kotesheni. *[Fomu ya mkataba pamoja na masharti yote ya malipo yanapaswa kutolewa kwa Fundi Mkazi pamoja na huu mwaliko wa Nukuu za bei/kotesheni ]*

15 Mafundi Wakazi wana haki ya kuomba kupitia upya maamuzi ya Ununuzi kulingana na **SEHEMU IX** ya Kanuni za Ununuzi katika Sekta ya Umma (Bidhaa, Kazi, Huduma Zisizo na Ushauri na Kitalaamu na Uuzaji wa Mali za Umma kwa Zabuni)- Tangazo la Serikali Na. 446 la Mwaka 2013 marekebisho 2016.

3. Fomu ya Kuwasilisha Nukuu za Bei/Kotesheni
4. Masharti Maalumu ya Mkataba
5. Masharti ya Jumla ya Mkataba
6. Maelezo ya Mahitaji, Viwango na Vipimo
7. Michoro
8. Mchanganuo wa Makadirio ya Kazi
9. Nyaraka nyingine zozote zinazounda sehemu ya mkataba (Kumbukumbu za ufafanuzi, memoranda dhidi ya rushwa)

**B: MAJUKUMU**

**Kifungu 7: Utekelezaji wa Kazi**

Fundi Mkazi atatoa nguvu kazi, zana , mitambo, usafiri, vifaa na cho chote kile kinachohitajika kwa ukamilishaji wa kazi. Atafanya kazi kulingana na inavyotakiwa na nyaraka za mkataba, na maelekezo ya ziada kama yatakayotolewa mara kwa mara.

**Kifungu 8: Hali Mbaya ya Ukinzani**

Iwapo wakati wa utekelezaji wa kazi Fundi Mkazi atapambana na halimbaya ya ukinzani ambayo haihusiani na hali ya hewa naambayo haikuwa imetabiriwa na Fundi Mkazi, Mhandisi atatathimini kuongeza muda ambaoFundi Mkazianastahili.

**Kifungu 9: Kutoa kazi kwa Fundi Msaidizi**

Fundi Mkazi hatatoa kazi au sehemu ya kazi kwa Fundi Mkazi msaidizibila kibali cha maandishi cha kutoka kwa Mwajiri. Kibali kama hicho kinapotolewa hakimwondolei Fundi Mkazi mamlaka au majukumu yake chini ya maktaba na hivyo Fundi Mkazi atakuwa na wajibu kwa kushindwa au kuzembea kwa Mafundi Wakazi wasaidizi.

**Kifungu 10: Usimamizi wa Kazi Unaofanywa na Fundi Mkazi**

Fundi Mkazi atatekeleza kazi kwa uangalifu na kwa kufuata utendaji unaotakiwa na Mhandisi ili kufikia mahitaji maalumu ya ubora, kiasi na muda uliopangwa. Kama katika wakati wowote ule Mhandisi anaona uzembe, au kubadilika sana kwa mwelekeo wa programu, hatua zinazofaa zitachukuliwa na Fundi Mkazi ili kurekebisha hali.

**Kifungu 11: Ukaguzi**

Mhandisi au mwakilishi wake aliyempa mamlaka ana haki ya kukagua kazi na Fundi Mkazi atatoa usaidizi kwa shughuli hiyo na kwa wakati Mhandisi atakapohitaji.

**Kifungu 12: Kazi Zinazokataliwa**

Kazi ambazo hazikuzingatia masharti ya mkataba zitakataliwa. Kwa maelekezo ya Mhandisi, Fundi Mkazi kwa gharama zake mwenyewe atatengeneza au kurekebisha au kufanya upya kazi itakayokataliwa hadi kumridhisha Mhandisi. au vifo.

**Kifungu13: Wajibu wa Fundi Mkazi**

Fundi Mkazi hatamhusisha Mwajiri dhidi ya madai yoyote yanayotokana na hasara au uharibifu wa upande wa tatu (third party). Atamkinga kikamilifu

Mwajiri wake dhidi ya madai au hasara zitakazotokana na Sheria ya Ajira na Fi ya Wafanyakazi.

**Kifungu14: Jambo Lisilozuilika**

Katika tukio la hasara yoyote au uharibifu unaotokea katika utendaji wa air yoyote wa nguvu za asili ambao pande za mkataba hazikuweza kufikiria mapem. Fundi Mkazi atarekebisha hasara au uharibifu. Mwajiri ataaamua kutoa ziada y Bei ya Mkataba na pia anaweza kufikiria kutoa muda wa nyongeza wa kipindi ch. mkataba.

**Kifungu15: Ubora wa Maunzi na Usanifu wa Kazi**

Maunzi yote na usanifu wa kazi vitakuwa na ubora kama ilivyofafanuliwa katika mkataba na pia kulingana na maelekezo ya Mhandisi na vitapimwa kama Mhandisi atakavyoona inafaa. Fundi Mkazi atatoa bure msaada unaohitajika kwa ajili ya kupima ubora wa maunzi na atakuwa na wajibu wa kugharimia upimaji wote utakaohitajika.

**Kifungu 16: Upatikanaji wa Maunzi**

Fundi Mkazi atabainisha vyanzo vyote vya maunzi yanavyohitajika kabla ya kuanza kwa kazi. Mwajiri akitakiwa anaweza kuwezesha upatikanaji wa vyanzo hivyo. Fundi Mkazi hatatumia maunzi bila kwanza kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Mhandisi.

**Kifungu17: Usafishaji wa Eneo la Kazi**

Baada ya kumaliza kazi, Fundi Mkazi ataondoa kutoka eneo la kazi zana zote, na maunzi ya ziada, uchafu na mitambo ya muda na ataacha eneo la kazi likiwa safi na katika hali itakayokubaliwa na Mhandisi.

**Kifungu18: Afya, Usalama na Kulinda Mazingira.**

Fundi Mkazi katika kipindi chote cha mkataba atakuwa na wajibu kamili ya kiafya na kiusalama katika eneo lake ya kazi na watu wote wanaopaswa kuwa katika eneo la kazi katika hali ya mpango mzuri ili kuepusha hatari kwa watu hao. Fundi Mkazi atazingatia mahitaji na kanuni zote za mazingira kama zinavyoelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kifungu19: Kuanza na Kukamilika kwa Kazi.**

Fundi Mkazi ataanza na kukamilisha kazi katika muda uliyoelezwa kwenye Masharti Maalumu ya Mkataba au katika kipindi cha mkataba cha nyongeza, kama kipindi hicho kimeruhusiwa na Mwajiri.

**Kifungu20: Mabadiliko ya Wigo wa kazi**

Kwa idhini ya Mwajiri, Mhandisi anaweza kubadilisha umbo, ubora au kiasi cha kazi na atakuwa na mamlaka ya kumwagiza Fundi Mkazi ipasavyo. Mabadiliko hayo yatafanywa kwa agizo la Mabadiliko katika Mkataba. Mhandisi ataamua kuhusu kiasi (kama itatokea) ambacho kwa maoni yake kinapaswa kuongezwa au kupunguzwa kutoka jumla ya fedha iliyotajwa kwenye Mkataba kwa ajili ya kazi yoyote ya nyongeza iliyofanywa au iliyoachwa kwa agizo hilo. Kiasi cha fedha kitakachoamuliwa kitatokana na kiwango cha kizio au kama hakuna kiwango cha kizio kinachotumika, kiwango kingine kitatumika kama itakavyoamriwa na Mhandisi na kukubaliwa na wote, Mwajiri na Mkandarasi.

## C: MALIPO

**Kifungu 21: Kiasi**

Kiasi kilichowekwa kwenye mchanganuo wa Makadirio ya Kazi ni kiasi kilichokadiriwa kwa kazi na kisichukuliwe kuwa ndiyo kiasi halisi sahihi kitakachofanywa na Fundi Mkazi.Mhandisi atapima thamani ya kazi halisi iliyofanyika na ataidhinisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika kama ilivyofafanuliwa katika mkataba. Ukomo wa kiasi cha kazi unaweza kuongezeka au kupungua kwa asilimia 10 ya bei ya mkataba na hii haitahitaji kibali cha Kamati za Usimamizi wa Miradi na Shule.

**Kifungu 22: Malipo**

**22.1 Malipo Wakati Kazi Inaendelea**

Malipo yatafanywa kwaFundi Mkaziwakati kazi inaendelea baada ya Mhandisi kutoa cheti kinachoonyesha kuwa kazi imekamilika kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba.

**22.2 Ucheleweshwaji wa Malipo**

Kama mwajiri atashindwa kufanya malipo katika muda uliotajwa, Mwajiri atamlipa Mkandarasi riba katika kiwango kilichotajwa kwenye **Masharti Maalumu ya Mkataba**.

**22.3 Makato ya Malipo**

Mwajiri atakuwa na haki ya kukata fedha kiasi cho chote kutoka kwa Fundi Mkazi kwenda kwa Mwajiri kutokana na fedha yoyote anayoweza kulipwa Fundi Mkazi na Mwajiri chini ya mkataba huu au mkataba mwingine ilimradi kifungu hiki hakitaathiri marekebisho yoyote kwa amri ya sheria au pengine Mwajiri anaweza kuwa na haki ya kurudishiwa fedha yoyote kama hiyo.

**22.4 Malipo kwa Wafanyakazi**

Kama kutatokea kushindwa kulipa mishahara/ujira na fidia nyingine zinazopaswa kulipwa wafanyakazi na /au malipo ya kukodisha mitambo/zana/magari na vifaa chini ya mkataba huu, mwajiri atakuwa na haki ya kushikilia malipo ya Fundi Mkazi.

Mwajiri atatumia fedha alizoshikilia kuwalipa wafanyakazi wa Fundi Mkazi mishahara yao na fidia nyingine na ada za kukodisha maunzi. Malipo kama hayo yatachukuliwa kuwa ni malipo yaliyopokelewa na Fundi Mkazi kutoka kwa Mwajiri chini ya mkataba huu.

**Kifungu 23: Malipo ya Ucheleweshaji kazi**

Kama Fundi Mkazi atashindwa kukamilisha kazi yake katika muda uliotajwa kwenye mkataba au katika muda wo wote wa nyongeza ulioruhusiwa na Mwajiri, Fundi Mkazi atamlipa Mwajiri malipo ya ucheleweshaji wa kazi katika kiwango cha asilimia 0.1 cha thamani ya mkataba kwa siku mpaka kiwango cha juu cha asilimia 10 ya bei ya mkataba.

## D: KUSULUHISHA MIGOGORO NA KUVUNJA MKATABA

### Kifungu 24: Kusuluhisha Migogoro

Kama migogoro ikitokea itasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote. Kam mazungumzo yatashindwa kuleta makubaliano, kilaupande una hiari ya kwend kwenye maamuzi kulingana na sheria za Tanzania.

### Kifungu 25: Uvunjaji wa Mkataba

25.1 Kama Fundi Mkazi anashindwa kuanza kazi katika muda uliopangwa au kuna sababu ya kutosha kuwa hatakamilisha kazi katika muda uliopangwa au kuna ucheleweshaji uliokiuka tarehe ya kukamilisha kazi au hayuko makini kufuata maelekezo yanayotolewa na Mhandisi au anakuwa mufilisi, Mwajiri atakuwa na haki ya kuvunja mkataba na kumwajiri Fundi Mkazi mwingine kufanya kazi hiyo.

25.2 Kama Mwajiri atashindwa kumlipa Fundi Mkazi katika muda wa siku 30 tangu tarehe ya cheti cha malipo kuidhinishwa na Mhandisi, Fundi Mkazi anaweza kuvunja mkataba.

### Kifungu 26: Malipo kama Mkataba Umevunjwa

Kama mkataba utavunjwa, Fundi Mkazi atalipwa na Mwajiri kiasi chafedha au vifaa ambavyo havitakuwa tayari vimelipiwa katika malipoyaliyofanywa kwa Fundi Mkazi kwa kazi zote zilizofanywa kabla ya tarehe ya kuvunjwa kwa mkataba kwa kiwango na bei inayotolewa kwenye mkataba. Kila malipo yoyote yanayofanywa na Mwajiri chini ya kifungu hiki, mwajiri atakuwa na haki ya kulipwamadeni yote kutokana na malipo ya awali aliyolipwa Fundi Mkazi kwaajili ya mitambo/zana/magari na maunzi na jumla yoyote ya fedha ambayo imelipwa hapo awali na Mwajiri kwenda kwa Fundi Mkazi kwa minajiri ya utekelezaji wa kazi.


## SEHEMU V: MASHARTI MAALUMU YA MKATABA

Taarifa maalumu ifuatayo kwa ajili ya kazi inayofanywa itakuwanyongeza, au inaweza kurekebisha vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba. Kunapokuwa na mgogoro, vifungu katika **Masharti Maalumu ya Mkataba** vitakuwa na nguvu zaidi ya vifungu katika **Masharti ya Jumla ya Mkataba**.

| Masharti Maalumu ya Mkataba Kifungu Na; | Masharti ya Jumla ya Mkataba Kifungu Na; | Marekebisho ya, na Nyongeza kwa vifungu katika Masharti ya Jumla ya Mkataba. |
|---|---|---|
| 1 | 19 | Mkataba unanza tarehe: …………… *na kumalizika tarehe*………………………….. |
| 2 | 19 | Muda wa kukamilisha ni *Siku Sitinii ( 60 )* |
| 3 | 23.0 | Malipo ya Ucheleweshaji kazi kwa 0.1 ya gharama ya kazi kwa siku |
| 4 | 23.1 | Asilimia ya fedha inayoshikiliwa ya Thamani ya cheti cha malipo (05%) |
| 5 | 23.2 | Ujenzi utakaguliwa na mhandisi wa manispaa ya Temeke |
| 6 | 23.3 | Kiwango cha riba kwa kiasi kisicholipwa ni kile kiwango cha riba kwa mwezi kinachotumiwa na benki ya biashara kama kilivyopitishwa na Benk kuu ya Tanzania tarehe ya kutia sahihi mkataba.(Hakuna) |
| 7 | 24 | Ucheleweshaji kazi kwa pande zotembili, 0.1% ya thamani ya pesa ya ufund kwa siku. |

# SEHEMU VI: MAELEZO YA MAHITAJI, VIWANGO NA VIPIMO

# SEHEMU VII: MICHORO




FLOOR PLAN (EMD)

Notes:
- THIS DRAWING IS COPYRIGHT
- DO NOT SCALE THIS DRAWINGS. ANY DESCREPANCIES TO BE REPORTED TO THE OFFICE OF CONSULTANT
- THIS DRAWING TO BE READ IN CONJUCTION WITH SPECIFICATIONS AND ALL OTHER DRAWINGS

N


Project Title:
PROPOSED RENOVATION / REFURBISHMENT OF EMD AND ICU BUILDING TO BE BUILT AT TEMEKE REGIONAL REFERRAL HOSPITAL, IN TEMEKE MUNICIPALITY.

Client:
TEMEKE REGIONAL REFERRAL HOSPITAL,
P.O.BOX
DAR ES SALAAV

Consultant:

MUNICIPAL ENGINEER
TEMEKE

| Tittle: | Floor plan |
|---|---|
| Drawn by : | |
| Checked by: | |
| Designed by: | |
| Scale: | 1 : 100 |
| Sheet No.: | |
| Date: | 2021 |




**ELEVATION**

N

Project Title:
PROPOSED RENOVATION / REFURBISHMENT OF EMD AND ICU BUILDING TO BE BUILT AT TEMEKE REGIONAL REFERRAL HOSPITAL, IN TEMEKE MUNICIPALITY

Client:
TEMEKE REGIONAL REFERRAL HOSPITAL,
P.O.BOX
DAR ES SALAAM

Consultant:

| | |
|---|---|
| Tittle: | ELEVATION |
| Drawn by: | |
| Checked by: | |
| Designed by: | |
| Scale: | 1 : 100 |
| Sheet No.: | |
| Date: | 2021 |

MUNICIPAL ENGINEER
TEMEKE

# SEHEMU VIII: FOMU MBALIMBALI

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA YA TEMEKE**

**Baruapepe: temekerh@afya.go.tz, S.L.P 45232 Dar es Salaam, Simu 0222856007**


## FOMU YA KUWASILISHA NUKUU YA BEI

*Tarehe:* 25/11/2021

**Kwa:** Mkurugenzi,

Hospitali ya rufaa ya mkoa Temeke,

S.L.P 45232,

DAR ES SALAAM.

Tunaahidi/Naahidi kutekeleza kazi ya ME/007/W/2021-2022/TMKRRH/LOT 02 kulingana na Masharti ya Mkataba yanayofuatana na Nukuu za Bei ya Mkataba...TZS Milioni Arobaini laki nane na elfu hamsini tu *[In giza kusi katika maneno* 40,850,000/= *tarakimu na aina ya sarafu]* Shilingi za Tanzania.

Pia tunaahidi kukamilisha kazi iliyotajwa katika kipindi cha WIKI 12........siku/wiki/miezi*(Futa visivyohitajika),* ambacho kinajumuisha kipindi cha maandalizi.

Nukuu za Bei hii pamoja na barua yako ya kukubali kwa maandishi vitafanya mkataba unaotufunga sisi pamoja. Tunafahamu kuwa hulazimiki kukubali kiwango cha chini au kotesheni yoyote kati ya kotesheni unazopokea.

Tunathibitisha kuwa kotesheni hii imetimiza masharti kama yanavyotajwa katika Mwaliko wa Nukuu za Bei.

Sahihi Idhinishwa: ........[signature]........

Jina na Cheo cha Mweka Sahihi: FUNDI MKAZI -DOP

Jina la Fundi Mkazi: ....TPFCS....

K.n.v: MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA POLISI (T)
S. L. P 79429
DAR ES SALAAM

## SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MEMORANDA KWA AJILI YA SERA DHIDI YA RUSHWA

Sisi ......TPFCS...... tunaweka umuhimu katika zabuni ya ushindani unaofanyika kwa misingi ya haki na huru na isiyoruhusu ukiukwaji wa taratibu na kanuni. Tunapenda kuthibitisha kuwa hatutatoa wala kuwezesha moja kwa moja au sivo moja kwa moja ushawishi usiofaa au zawadi kwa ofisa yeyote wa umma, ndugu zake au watu wenye uhusiano wa kibiashara, kuhusiana na kotesheni hii au baadaye katika utekelezaji wa mkataba kama tutafanikiwa.

Tunayo Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu inayojumuisha hatua zote muhimu na za kutosha kuhakikisha kuwa ahadi yetu ya kutotoa rushwa iliyotolewa katika maelezo haya itazingatiwa na menejimenti yetu na waajiriwa na pia watu wengine wote wanaofanya kazi nasi katika miradi ya sekta ya umma au mkataba ikiwa ni pamoja na wakala, washauri, wabia wetu, wakandarasi wasaidizi na watoa huduma wetu. Nakala zetu za Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya ukubalifu zimeambatishwa.

FRANCIS D. SUKA
*(Jina la mtu aliyepewa mamlaka)*

*Sahihi* [signature]

25/11/2021

*Tarehe*

K.n.y: MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA POLISI (T)
S. L. P 79429
DAR ES SALAAM

*Muhuri/ Alama ya Kampuni (Kama ipo)*